JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA WA KIDATO CHA NNE NA MAARIFA ULIOFANYIKA NOVEMBA 2023

**IMETOLEWA NA:**

**KATIBU MTENDAJI**
**TAREHE : 25 JANUARI 2024**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika Mkutano wake wa **158** uliofanyika tarehe **22 Januari**, **2024**, Baraza la Mitihani la Tanzania liliidhinisha kutangazwa rasmi kwa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa uliofanyika mwezi Novemba, 2023.

## 2.0 USAJILI NA MAHUDHURIO

### 2.1 Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne

#### (a) Watahiniwa Wote

Jumla ya watahiniwa **572,359** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne wakiwemo Wasichana **310,248** (**54.21%**) na Wavulana **262,111** (**45.79%**). Kati ya watahiniwa **572,359** waliosajiliwa, watahiniwa wa Shule walikuwa **543,332** na watahiniwa wa Kujitegemea walikuwa **29,027**.

#### (b) Watahiniwa wa Shule

Kati ya watahiniwa **543,332** wa Shule waliosajiliwa, watahiniwa **529,596** sawa na asilimia **97.47** walifanya mtihani ambapo Wasichana walikuwa **284,893** (**97.19%**) na Wavulana **244,703** (**97.80%**). Watahiniwa **13,736** sawa na asilimia **2.53** hawakufanya Mtihani.

#### (c) Watahiniwa wa Kujitegemea

Kati ya watahiniwa **29,027** wa Kujitegemea waliosajiliwa, watahiniwa **25,626** sawa na asilimia **88.28** walifanya Mtihani na watahiniwa **3,401** sawa na asilimia **11.72** hawakufanya Mtihani.

### 2.2 Mtihani wa Maarifa

Jumla ya watahiniwa **10,953** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Maarifa wakiwemo Wanawake **6,920** sawa na asilimia **63.18** na Wanaume **4,033** sawa na asilimia **36.82**. Kati ya Watahiniwa waliosajiliwa, watahiniwa **8,630** walifanya Mtihani wa Maarifa, wakiwemo Wanawake **5,343** (**77.21%**) na Wanaume **3,287** (**81.50%**). Watahiniwa **2,323** sawa na asilimia **21.21%** hawakufanya Mtihani.

# 3.0 MATOKEO

## 3.1 Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne

### 3.1.1 Ufaulu wa Ujumla

#### (a) Watahiniwa Wote

Jumla ya watahiniwa **484,823** sawa na asilimia **87.65** ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne 2023 wamefaulu. Wasichana waliofaulu ni **257,892** sawa na asilimia **86.17** wakati Wavulana waliofaulu ni **226,931** sawa na asilimia **89.40**. Mwaka 2022 watahiniwa waliofaulu walikuwa ni **476,450** sawa na asilimia **86.78**. Hivyo, ufaulu wa watahiniwa **umeongezeka** kwa asilimia **0.87** ikilinganishwa na mwaka 2022.

#### (b) Watahiniwa wa Shule

Jumla ya watahiniwa wa Shule **471,427** kati ya **527,576** wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia **89.36** wamefaulu ambapo wamepata Madaraja ya **I**, **II**, **III** na **IV**. Mwaka 2022 Watahiniwa waliofaulu walikuwa **456,975** sawa na asilimia **87.79**. Hivyo, ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **1.57**. Aidha, kuna ongezeko la watahiniwa **14,452** sawa na asilimia **3.16** ya waliofaulu ikilinganishwa na mwaka 2022.

Kati ya watahiniwa **471,427** waliofaulu, Wasichana ni **250,147** sawa na asilimia **88.11** na Wavulana ni **221,280** sawa na asilimia **90.81**. Hivyo, Wavulana wamefaulu vizuri zaidi kuliko Wasichana.

#### (c) Watahiniwa wa Kujitegemea

Watahiniwa wa Kujitegemea waliofaulu mtihani ni **13,396** sawa na asilimia **52.44**. Mwaka 2022 Watahiniwa wa Kujitegemea **19,475** sawa na asilimia **68.34** walifaulu mtihani huo. Hivyo, ufaulu wa Watahiniwa wa Kujitegemea **umeshuka** kwa asilimia **15.90** ikilinganishwa na mwaka 2022.

### 3.1.2 Ubora wa Ufaulu

Ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata watahiniwa wa Shule unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri wa Madaraja ya **I - III** ni **197,426** sawa na asilimia **37.42**. Mwaka 2022 watahiniwa waliopata ufaulu wa madaraja I - III walikuwa **192,348** sawa na asilimia **36.95**. Hivyo, ubora wa ufaulu **umeongezeka** kwa asilimia **0.47** ikilinganishwa na mwaka 2022.

Ubora wa ufaulu wa Madaraja ya **I - III** ni mzuri zaidi kwa Wavulana ikilinganishwa na Wasichana ambapo Wavulana ni **108,368** (**44.47%**) na Wasichana ni **89,058** (**31.37%**). Mchanganuo wa ufaulu katika madaraja mbalimbali umeainishwa katika Jedwali Na.**1**.

**Jedwali Na.1: Ufaulu wa Jumla Kimadaraja kwa Watahiniwa wa Shule**

| Daraja | Mwaka | Wavulana | | Wasichana | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| I | 2022 | 22,038 | 9.14 | 15,699 | 5.62 | 37,737 | 7.25 |
| | 2023 | 24,717 | 10.14 | 17,731 | 6.25 | 42,448 | 8.05 |
| II | 2022 | 37,484 | 15.54 | 30,555 | 10.94 | 68,039 | 13.07 |
| | 2023 | 39,804 | 16.34 | 31,451 | 11.08 | 71,255 | 13.51 |
| III | 2022 | 45,728 | 18.96 | 40,844 | 14.62 | 86,572 | 16.63 |
| | 2023 | 43,847 | 17.99 | 39,876 | 14.05 | 83,723 | 15.87 |
| **I - III** | **2022** | **105,250** | **43.64** | **87,098** | **31.18** | **192,348** | **36.95** |
| | **2023** | **108,368** | **44.47** | **89,058** | **31.37** | **197,426** | **37.42** |
| IV | 2022 | 108,440 | 44.96 | 156,187 | 55.91 | 264,627 | 50.84 |
| | 2023 | 112,912 | 46.34 | 161,089 | 56.74 | 274,001 | 51.94 |
| **I - IV** | **2022** | **213,690** | **88.60** | **243,285** | **87.08** | **456,975** | **87.79** |
| | **2023** | **221,280** | **90.81** | **250,147** | **88.11** | **471,427** | **89.36** |
| 0 | 2022 | 27,502 | 11.40 | 36,081 | 12.92 | 63,583 | 12.21 |
| | 2023 | 22,385 | 9.19 | 33,764 | 11.89 | 56,149 | 10.64 |

### 3.1.3 Ufaulu wa Shule katika Makundi ya Umahiri

Ufaulu katika makundi ya Umahiri unaonesha kuwa, kati ya shule zote **5,343** zenye matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne 2023, shule **5,334** (**99.83%**) zimepata wastani wa Daraja la **A-D** ikilinganishwa na shule **5,169** (**99.58%**) zilizopata wastani wa madaraja hayo mwaka 2022. Hivyo,

wastani wa Daraja la **A-D**.

Shule zilizopata wastani wa Daraja la **A-C zimeongezeka** kwa asilimia **1.36** kutoka idadi ya shule **1,870** (**36.02%**) mwaka 2022 hadi kufikia idadi ya shule **1,997** (**37.38%**) mwaka 2023. Mchanganuo zaidi umebainishwa katika Jedwali Na. **2**.

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Shule katika Makundi ya Umahiri kwa Mwaka 2023 ikilinganishwa na Mwaka 2022**

| Daraja | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | % | Idadi | % |
| A | 85 | 1.64 | 97 | 1.82 |
| B | 500 | 9.63 | 565 | 10.57 |
| C | 1,285 | 24.75 | 1,335 | 24.99 |
| D | 3,299 | 63.55 | 3,337 | 62.46 |
| F | 22 | 0.42 | 9 | 0.17 |

### 3.1.4 Ufaulu wa Watahiniwa Kimasomo

#### 3.1.4.1 Masomo ya Sayansi Jamii

Watahiniwa waliofaulu masomo ya **Civics**, **History** na **Geography** ni kati ya asilimia **63.20** hadi **67.83**. Katika somo la **History** ufaulu umeongezeka kwa asilimia **1.19** na umeshuka kwa asilimia **2.21** kwenye somo la **Civics** na asilimia **1.78** kwenye somo **Geography** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.

Masomo ya Sayansi Jamii yana ubora wa ufaulu wa kati ya asilimia **30.33** hadi **30.91** kwa watahiniwa waliopata ufaulu kati ya gredi **A** hadi **C** sawa na alama **45** hadi **100**. Ufaulu ya watahiniwa waliopata Gredi **A** na **B** umeongezeka kwa asilimia **1.94** kwenye somo la **Civics**, asilimia **1.07** kwenye somo la **History** na asilimia **1.51** kwenye somo la **Geography** ikilinganishwa na mwaka 2022. Aidha, watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** kwenye masomo ya Sayansi Jamii ni kati ya asilimia **5.26** hadi **7.01**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Sayansi Jamii umeoneshwa katika Jedwali Na. **3**.

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Civics | 2022 | 520,393 | 0.77 | 4.32 | 31.45 | 70.04 | 29.96 |
| | 2023 | 527,671 | 1.71 | 6.26 | 30.91 | 67.83 | 32.17 |
| History | 2022 | 509,356 | 1.66 | 5.94 | 30.37 | 62.01 | 37.99 |
| | 2023 | 517,051 | 2.18 | 7.01 | 30.48 | 63.20 | 36.80 |
| Geography | 2022 | 519,271 | 0.62 | 3.75 | 32.33 | 66.10 | 33.90 |
| | 2023 | 526,789 | 1.27 | 5.26 | 30.33 | 64.32 | 35.68 |

#### 3.1.4.2 Masomo ya Lugha

Masomo ya **Kiswahili** na **Chinese Language** yana ufaulu mzuri sana ambapo watahiniwa waliofaulu somo la Kiswahili ni asilimia **96.80** na somo la **Chinese Language** ni asilimia **91.36**. Ufaulu wa masomo ya **English Language**, **Literature in English** na **French Language** ni mzuri ambapo watahiniwa waliofaulu somo la English Language ni asilimia **69.09** na katika masomo ya **Literature in English** na **French Language** watahiniwa waliofaulu ni kati ya asilimia **79.34** na **79.56**. Aidha, somo la **Arabic Language** ufaulu unaendelea kuimarika kutoka asilimia **24.58** kwa mwaka 2022 hadi **26.83** kwa mwaka 2023.

Somo la **Kiswahili** lina ubora wa ufaulu wa asilimia **74.39** na katika masomo ya **English Language**, **Literature in English**, **French Language** na **Chinese Language** yana ubora wa ufaulu wa kati ya asilimia **27.33** hadi **54.09** kwa watahiniwa waliopata ufaulu wa kati ya gredi **A** hadi **C** sawa na alama **45** hadi **100**.

Ufaulu wa watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** umeongezeka kwa asilimia **1.54** kwenye somo la **Kiswahili** na umeshuka kwa kati ya asilimia **0.02** hadi **1.26** kwenye masomo ya **English Language**, **Literature in English** na **Arabic Language**. Katika somo la **French Language** na **Chinese Language** asilimia ya waliopata gredi **A** na **B** imeshuka kati ya

2022.

Aidha, watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** kwenye masomo ya Lugha ni kati ya asilimia **1.86** hadi **19.09** ambapo somo la **Chinese Language** lina asilimia **19.09**, likifuatiwa na somo la **Kiswahili** lenye asilimia **18.87**, somo la **Literature in English** lenye asilimia **5.90** na somo la **English Language** lenye asilimia **5.41**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Lugha umeoneshwa katika Jedwali Na. **4**.

**Jedwali Na. 4: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Lugha**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | 2022 | 520,501 | 3.54 | 17.33 | 73.84 | 95.58 | 4.42 |
| | 2023 | 527,708 | 4.25 | 18.87 | 74.39 | 96.80 | 3.20 |
| English Language | 2022 | 520,478 | 2.64 | 6.67 | 28.83 | 68.72 | 31.28 |
| | 2023 | 527,672 | 1.34 | 5.41 | 27.49 | 69.09 | 30.91 |
| French Language | 2022 | 2560 | 2.81 | 8.32 | 32.27 | 75.63 | 24.38 |
| | 2023 | 2,338 | 0.81 | 3.64 | 27.33 | 79.56 | 20.44 |
| Literature in English | 2022 | 109,029 | 1.29 | 6.63 | 42.52 | 80.06 | 19.94 |
| | 2023 | 114,727 | 0.87 | 5.90 | 42.40 | 79.34 | 20.66 |
| Arabic Language | 2022 | 16,493 | 0.56 | 1.88 | 8.52 | 24.58 | 75.42 |
| | 2023 | 14,609 | 0.64 | 1.86 | 8.88 | 26.83 | 73.17 |
| Chinese Language | 2022 | 309 | 16.50 | 37.22 | 75.40 | 95.79 | 4.21 |
| | 2023 | 440 | 6.14 | 19.09 | 54.09 | 91.36 | 8.64 |

#### 3.1.4.3 Masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia

Ufaulu wa masomo ya **Physics**, **Chemistry**, **Biology**, **Engineering Science**, **Agriculture**, **Information and Computer Studies**, **Additional Mathematics** na **Food and Human Nutrition** ni kati ya asilimia **70.09** hadi asilimia **100** ambapo ufaulu wa juu upo katika somo la **Food and Human Nutrition** ambalo watahiniwa wote waliofanya somo hilo wamefaulu likifuatiwa na somo la **Additional Mathematics** asilimia **97.84**, somo la **Chemistry** asilimia **96.14**, somo la **Information and Computer Studies** asilimia **89.88** na somo la **Agriculture**

Aidha, ufaulu wa masomo ya **Physics**, **Chemistry**, **Biology**, **Engineering Science**, **Food and Human Nutrition** na **Basic Mathematics** umepanda kati ya asilimia **0.17** hadi **10.30**. Aidha, ufaulu wa somo la **Agriculture**, **Information and Computer Studies** na **Additional Mathematics** umeshuka kwa kati ya asilimia **1.64** hadi **5.60** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.

Masomo ya **Chemistry**, **Information and Computer Studies**, **Additional Mathematics** na **Food and Human Nutrition** yana ubora wa ufaulu wa kati ya asilimia **70.15** hadi **99.38** na katika masomo ya **Physics**, **Biology**, **Agriculture** na **Engineering Science** yana ubora wa ufaulu wa kati ya asilimia **32.82** hadi **58.55** kwa watahiniwa waliopata ufaulu wa kati ya gredi **A** hadi **C** sawa na alama **45** hadi **100**. Aidha, somo la Basic Mathematics lina ubora wa ufaulu wa asilimia **12.75**.

Ufaulu wa watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** umeongezeka kwa kati ya asilimia **0.03** hadi **26.34** katika masomo ya **Physics**, **Chemistry**, **Engineering Science**, **Information and Computer Studies**, **Basic Mathematics** na **Food and Human Nutrition** na umeshuka kwa kati ya asilimia **2.63** hadi **4.84** kwenye masomo ya **Biology**, **Agriculture** na **Additional Mathematics** ikilinganishwa na mwaka 2022.

Aidha, watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** kwenye masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia ni kati ya asilimia **4.11** hadi **58.50** ambapo somo la **Food and Human Nutrition** lina asilimia **58.50** likifuatiwa na somo la **Additional Mathematics** lenye asilimia **35.01** na somo la **Chemistry** lenye asilimia **30.01**. Somo la **Basic Mathematics** ni somo lenye ufaulu wa chini kwa watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** kwenye masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia japokuwa ni somo lenye asilimia kubwa ya watahiniwa waliopata gredi **A** ikilinganishwa na masomo ya **Physics**,

**English**, **Arabic Language**, **Commerce**, **Book-Keeping**, **Music**, **Physical Education**, **Theatre Arts** na baadhi ya masomo ya ufundi kama vile **Building Construction** na **Electronics and Communications Engineering**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia umeoneshwa katika Jedwali Na. **5**.

**Jedwali Na. 5: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Sayansi Asilia, Hisabati na Teknolojia**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Physics | 2022 | 114,144 | 0.46 | 3.10 | 27.04 | 68.34 | 31.66 |
| | 2023 | 121,644 | 1.03 | 5.03 | 32.82 | 71.85 | 28.15 |
| Chemistry | 2022 | 155,007 | 6.98 | 21.39 | 68.21 | 93.68 | 6.32 |
| | 2023 | 162,026 | 10.67 | 30.01 | 77.82 | 96.14 | 3.86 |
| Biology | 2022 | 520,399 | 4.13 | 10.68 | 36.54 | 67.84 | 32.16 |
| | 2023 | 527,574 | 2.24 | 8.05 | 35.36 | 70.09 | 29.91 |
| Agriculture | 2022 | 6,882 | 1.99 | 9.65 | 65.52 | 94.09 | 5.91 |
| | 2023 | 6,820 | 1.36 | 5.63 | 49.46 | 88.49 | 11.51 |
| Engineering Science | 2022 | 1,435 | 1.46 | 8.50 | 43.62 | 74.63 | 25.37 |
| | 2023 | 1,573 | 9.35 | 22.95 | 58.55 | 84.93 | 15.07 |
| Information and Computer Studies | 2022 | 3,065 | 7.08 | 23.10 | 70.41 | 91.52 | 8.48 |
| | 2023 | 3,517 | 8.56 | 26.16 | 70.15 | 89.88 | 10.12 |
| Basic Mathematics | 2022 | 520,332 | 2.16 | 4.08 | 10.76 | 20.08 | 79.92 |
| | 2023 | 527,608 | 1.84 | 4.11 | 12.75 | 25.42 | 74.58 |
| Additional Mathematics | 2022 | 394 | 18.53 | 39.85 | 89.34 | 99.75 | 0.25 |
| | 2023 | 417 | 15.83 | 35.01 | 78.90 | 97.84 | 2.16 |
| Food and Human Nutrition | 2022 | 2,301 | 3.39 | 32.16 | 94.92 | 99.83 | 0.17 |
| | 2023 | 2,241 | 13.43 | 58.50 | 99.38 | 100.00 | 0.00 |

Watahiniwa waliofaulu somo la **Commerce** ni asilimia **81.02** na waliofaulu somo la **Book-Keeping** ni asilimia **78.62**. Aidha, ufaulu wa somo la **Commerce** umeshuka kwa asilimia **2.90** na ufaulu wa somo la **Book-Keeping** umeshuka kwa asilimia **8.31**.

Somo la **Commerce** lina ubora wa ufaulu wa asilimia **37.81** na somo la **Book-Keeping** lina ubora wa ufaulu wa asilimia **38.83** kwa watahiniwa waliopata ufaulu wa kati ya gredi **A** hadi **C** sawa na alama **45** hadi **100**.

Aidha, watahiniwa waliopata gredi **A** na **B** kwenye somo la **Commerce** ni asilimia **4.70** na katika somo la **Book-Keeping** ni asilimia **6.75**. Mchanganuo wa ufaulu katika masomo ya Biashara umeoneshwa katika Jedwali Na. **6**.

**Jedwali Na. 6: Asilimia ya Ufaulu katika Masomo ya Biashara**

| SOMO | MWAKA | IDADI | % waliopata A [75-100] | % waliopata A hadi B [65-100] | % waliopata A hadi C [45-100] | % waliopata A hadi D [30-100] | % waliopata F [0-29] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Commerce | 2022 | 12,633 | 1.77 | 8.87 | 48.13 | 83.92 | 16.08 |
| | 2023 | 13,544 | 0.75 | 4.70 | 37.81 | 81.02 | 18.98 |
| Book-Keeping | 2022 | 12,060 | 4.67 | 13.35 | 53.82 | 86.93 | 13.07 |
| | 2023 | 13,203 | 1.67 | 6.75 | 38.83 | 78.62 | 21.38 |

### 3.1.4.5 Masomo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Ufaulu wa somo la **Fine Art**, **Music** na **Physical Education** ni mzuri ambao ni kati ya asilimia **87.40** hadi **97.76**. Aidha, somo la **Theatre Arts** lina ufaulu wa wastani ambao ni asilimia **58.39**. Ufaulu wa masomo ya **Fine Art**, **Music** na **Physical Education** umepanda kwa kati ya asilimia **5.01** hadi **14.05** na umeshuka kwa asilimia **26.65** katika somo la **Theatre Arts** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022.